Sheria ni agizo la shuruti linalotolewa na mamlaka kuu…, na KANUNI ni mwongozo au utaratibu maalumu unaotolewa kuhusiana na utekelezaji wa sheria iliyowekwa au agizo lililotolewa..

Kwamfano katika biblia kulikuwa na Sheria ya “kuishika  Pasaka” lakini ilikuwepo pia kanuni *(ambayo ni mwongozo wa namna ya kuiadhimisha hiyo siku),* kwamba ni lazima kwanza iwe *siku  ya 14* ya mwezi wa kwanza wa kalenda ya kiyahudi, na pia siku hiyo ni lazima achinjwe mwana kondoo na kumwoka motoni na aliwe pamoja na mboga zenye uchungu n.k *(Soma Kutoka 12:1-12).*

Sasa huo mwongozo wote wa jinsi ya kuiadhimisha hiyo siku ndio unaoitwa Kanuni, lakini sheria ni hiyo moja tu kwamba Waishike Pasaka..

> *Hesabu 9:14 “Na kama mgeni akiketi kati yenu ugenini, naye ataka kuishika Pasaka kwa Bwana; kama HIYO SHERIA YA PASAKA ILIVYO, na kama amri yake ilivyo, ndivyo atakavyofanya; MTAKUWA NA SHERIA MOJA, kwa huyo aliye mgeni, na kwa huyo aliyezaliwa katika nchi”.*

Katika biblia kila Amri au sheria ilikuwa na Kanuni zake na hukumu zake.

Tunayo sheria na amri ya Kristo pia ambayo ni UPENDO, lakini huu upendo unao kanuni…ni lazima tuzitafute kanuni za upendo na tuzijue.

> *Isaya 28:13 "Kwa maana ni amri juu ya amri, amri juu ya amri; kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni; huku kidogo na huku kidogo".*

Maran atha!

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kubofya link hii >>

https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10[1]

Kwa mawasiliano: +255693036618 au +255789001312

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

Kwanini tarehe ya pasaka inabadilika kila mwaka?[2]

PASAKA NI NINI? NA JE TUNARUHUSIWA KUSHEHEREKEA?[3]

Nini tofauti kati ya kileo na divai?[4]

FAHAMU MAISHA YA YESU KABLA YA HUDUMA.[5]

Je! kuna mwanamke mwingine aliyempaka Bwana marhamu (manukato) zaidi ya Mariamu ndugu yake Lazaro?[6]

Share on:
WhatsApp
Endnotes:

1. https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10: https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10

2. Kwanini tarehe ya pasaka inabadilika kila mwaka?: https://wingulamashahidi.org/2024/03/27/kwanini-tarehe-ya-pasaka-inabadilika-kila-mwaka/
3. PASAKA NI NINI? NA JE TUNARUHUSIWA KUSHEHEREKEA?: https://wingulamashahidi.org/2020/03/31/pasaka-ni-nini-na-je-tunaruhusiwa-kusheherekea-pasaka/
4. Nini tofauti kati ya kileo na divai?: https://wingulamashahidi.org/2025/02/24/nini-tofauti-kati-ya-kileo-na-divai/
5. FAHAMU MAISHA YA YESU KABLA YA HUDUMA.: https://wingulamashahidi.org/2023/04/03/fahamu-maisha-ya-yesu-kabla-ya-huduma/
6. Je! kuna mwanamke mwingine aliyempaka Bwana marhamu (manukato) zaidi ya Mariamu ndugu yake Lazaro?: https://wingulamashahidi.org/2023/05/03/je-kuna-mwanamke-mwingine-aliyempaka-bwana-marhamu-manukato-zaidi-ya-mariamu-ndugu-yake-lazaro/